Katika Jina Lako Tunatoa Utukufu
(Unto Thy Name Give Glory)

Na

Terry Warford

Katika Jina Lako Tunatoa Utukufu
(Unto Thy Name Give Glory)

Na

Terry Warford

Novemba 12, 2011

Katika Jina Lako Tunatoa Utukufu

Zaburi 115 ni kifungu kizuri cha andiko, ambayo tunatoa kwa ajili ya kukufurahisha na kujifunza kwako leo. Inavuvia. Huchanganua nguvu iliyo katika uwezo wa Mungu na uharibifu wa dunia. Inaahidi msaada, kinga na Baraka kutoka kwa Mungu kama tutamwamini na kutembea katika njia zake. Inahitimisha na sifa.

Hebu twende hatua kwa hatua katika Zaburi hii. Ndani yake tunakuta misaada inayotusaidia kuishi maisha ya Ukristo chini ya Agano Jipya, pamoja na ulinganifu kati ya vikwazo walivyokumbana navyo wakati ule na kile tunachokumbana nacho leo. Na hivyo Zaburi hii ya agano la kale bado inatupa somo lenye thamani ambayo twaweza kutumia chini ya Agano Jipya.

Zab. 115:1 hutambulisha zaburi kwa sifa, ikielekeza akili zetu kwa Mungu. "*Ee BWANA kutukuza usitutukuze sisi, bali ulitukuze jina lako, kwa ajili ya fadhili zako, kwa ajili ya uaminifu wako.*"

Mungu ni muhimu katika maisha yetu. Tunapaswa kukumbuka hilo kila siku tunapoamka, na kumtazama siku nzima. Yeye ni nambari moja. Tunapaswa kumheshimu na kumtumikia kila siku.

Hata chini ya Agano Jipya tunapaswa kuwa na uhakika katika kumsifu na kumtukuza. Katika sura ya 14 ya kitabu cha Matendo, wakati watu walitaka kuwaheshimu Paulo na Barnaba kama miungu, waliweka ukomo mara moja, na kuanza kuwageuza watu kwa Mungu wa Kweli. Mdo. 14:14-15, "*Walakini mitume Barnaba na Paulo, walipopata habari, wakararua nguo zao wakaenda mbio wakaingia katika makutano wakipiga kelele, wakisema akina bwana, mbona mnafanya haya? Sisi nasi tu wanadamu hali moja na ninyi; twawahubiri habari njema, ili mgeuke na kuyaacha mambo haya ya ubatili na kumwelekea Mungu aliye hai, aliyeumba mbingu na nchi na bahari na vitu vyote vilivyomo;*"

Matendo pamoja na maneno yetu yanapaswa kuwa katika utukufu wa Mungu, na sio yetu binafsi. Katika **Mat. 15:14-16**, Yesu alisema,

Lakini angalia mwandishi katika zaburi 115 hakuwa tu anatoa maisha yake kwa utukufu wa Mungu. Kimsingi alikuwa namuuliza Mungu kutukuza jina lake mwenyewe. "*…ulitukuze jina lako.*" Na katika Yohana 12:27-28, wakati Yesu alimwomba Mungu kwa kitu icho hicho, Mungu akatuhakikishia kwamba amelitukuza jina lake, na ataendelea kufanya hivyo. "*Sasa roho yangu imefadhaika nami nisemeje? Baba uniokoe katika saa hii? Lakini ni kwa ajili ya*

hayo nilivyoifikia saa hii. Baba ulitukuze jina lako. Basi ikaja sauti kutoka mbinguni. Nimelitukuza, name nitalitukuza tena."

Sehemu ya mwisho ya zaburi 115:1 inatoa sababu mbili za Mungu kulitukuza jina lake: "*…kwa ajili ya fadhili zako, kwa ajili ya uaminifu wako.*" Huruma na uaminifu siyo thamani katika msuguano. Hufanya kazi pamoja, uhitaji kila mmoja, na hupatikana katika maandiko. Zab. 85:10, inasema, "*Fadhili na kweli zimekutana, haki na amani zimehusiana.*" Vile vile hata leomaandiko ya Agano Jipya hutuambia kuzitumia vyote. Hazipo katika utenganifu. Ebr. 12:14, "*Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote na huo utakatifu, ambaye hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nayo.*"

Zaburi iliyobaki huchanganua sababu nyingi ni kwa nini utukufu ni wa Mungu.

Sehemu inayofuata hulinganisha nguvu ya Mungu na uharibifu wa dunia. Kumbuka kwamba juhudi zetu ni tofauti leo. Bali wao juhudi zao zilikuwa na ibada ya sanamu. Vita yetu kubwa leo ni dhidi ya wale wasio mwamini Mungu ao ambao wanataka kumwabudu kwa njia zao wenyewe kuliko zake. Lakini suluhisho letu hufanana na wale – kuamini katika Mungu wa kweli na aishiye.

Zab. 115:2-9, "*Kwa nini mataifa kusema yuko wapi Mungu wao? Lakini Mungu wetu yuko mbinguni alitakalo lote amelitenda. Sanamu zao ni fedha na dhahabu, kazi ya mikono ya wanadamu. Zina vinywa lakini hazisemi, zina macho lakini hazioni, zina masikio lakini hazisikii, zina pua lakini hazisikii harufu, mikono lakini hazishiki, miguu lakini haziendi, wala hazitoi sauti kwa koo zake. Wazifanyao wanafanana nazo, kila mmoja anayezitumainia. Enyi Israeli mtumainini BWANA; yeye ni msaada wao na ngao yao.*"

Leo hii, badala ya wao kuabudu miungu, kikundi ambacho kinasauti dhidi ya Mungu ni wale wasio mwamini. Siwezi kuona sehemu yo yote ya uumbaji wa Mungu bila ya kupigwa na ubumbuazi kuhusiana na ubunifu wake wa thamani. Ubunifu unahitaji mbunifu. Ni rahisi na ni kweli. **Ebr. 13:4,** Wale wanaochagua kutokuamini ukweli huo wa wazi wanafanya hivyo kwa sababu hawataki kufuata maagizo yake. Zab. 14:1, "*Mpumbavu amesema moyoni, hakuna Mungu; wameharibu matendo yao na kuyafanya chukizo, hakuna atendaye mema.*"

Kumwamini Mungu Muumba wetu na Bwana, kwa nini tunaabudu na kumtumikia Mungu kwa njia yo yote isipokuwa kwa njia anayoitaka? Bado hutokea miongoni mwetu. Yesu aliuliza swali hili katika Luka 6:46, "*Kwa nini mnaniita Bwana, Bwana, wakati hamyatendi niwaamuruyo?*"

Kama Israeli katika siku zile, leo tunashinda kupitia kumwamini Bwana, 2 Tim. 1:12, "*Kwa sababu hiyo* (kuhubiri injili, msitari wa 11) *nimepatikana na mateso haya wala sitahayari; kwa maana namjua yeye niliyemwamini, na kusadiki ya kwamba aweza kukilinda kile nilichokiweka amana kwake hata siku ile.*"

Sehemu inayofuata la somo letu inaendeleza fikra hii ya kumwanini Mungu, na inatupa sababu kadhaa za kumwamini. Zab. 115:10-16, "*Enyi mlango wa Haruni, mtumainini BWANA; yeye ni msaada wao na ngao yao. Enyi mmchao BWANA, mtumainini BWANA, yeye ni msaada wao na ngao yao. BWANA ametukumbuka, naye atatubariki sisi. Ataubariki mlango wa Israeli, ataubariki mlango wa Haruni, atawabariki wamchao BWANA, wadogo kwa wakubwa. BWANA na awaongoze ninyi, ninyi na watoto wenu. Na mbarikiwe ninyi nna BWANA, aliyezifanya bingu na nchi. Mbingu ni mbingu za BWANA, bali nchi amewapa wanadamu.*" Hebu tuangalie mambo kadhaa katika kifungu hiki.

Kwanza, tunaposoma kuhusu nyumba ya Israeli hapa, elewa kwamba kanisa ndio Israeli ya leo. Rum. 2:28-29, "*Maana yeye si Myahudi aliye Myahudi kwa nje tu, wala tohara siyo ile ya nje tu katika mwili; bali yeye ni Myahudi aliye Myahudi kwa ndani na tohara ni ya moyo, katika roho si katika andiko; ambaye sifa yake haitoki kwa wanadamu bali kwa Mungu.*"

Tuna sababu nzuri ya kumwogopa Bwana, kama inavyoamuriwa hapa. Yesu alisema katika Mat. 10:28, "*Msiwaogope wauao mwili wasiweze kuiua na roho, afadhali mwogopeni Yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum.*"

Lakini pia mwandishi wetu ametaja kwamba Mungu wetu pamoja na uwezo mkuu anafanya kazi kwa niaba yetu. Mara tatu katika mistari ya 9-11 ya Zab. 115, ametaja kwamba Mungu ndiye msaada wetu na ngao. Msitari wa 11 inasema, "*Enyi mmchao BWANA, mtumainini BWANA; yeye ni msaada wao na ngao yao.*" Anaendelea na kusema kwamba Mungu ametubariki, katika kutubariki, na ataendelea kutubariki. Vile vile tunaendelea kusoma Baraka zake kuu katika maandiko ya Agano Jipya. Fil. 4:19, "*Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristo Yesu.*"

Mungui ana nguvu zote, na yuko upande wetu. Nikirudia wazo zuri ya Zab. 115:15, "*Mmebarikiwa na BWANA aliyezifanya mbingu na dunia.*"

Mistari miwili ya mwisho ya Zab. 115 inatuambia kwamba hata ivyo wengine hawamtukuzi Bwana, bali sisi tutamtukuza. Zab. 115: 17-18, "*Sio wafu wamsifuo BWANA, wala wo wote washukao*

kwenye kimya. Bali sisi tutamhimidi BWANA, tangu leo na hata milele."

Ninakumbushwa kuhusu wimbo "Tunakwenda Sayuni". Hakika, kunawale ambao wanakataa kuimba, na hiyo ni huzuni kwa sababu hakika wamekufa. Lakini acha wakatae kama wakitaka. Usiruhusu kukataa kwao au mateso yao yatuzuie kumwimbia Mungu nyimbo za sifa. Ebr. 13:15, "*Basi kwa njia yake yeye, na tumpe Mungu dhabihu ya sifa daima, yaani tunda la midomo iliungamayo jina lake.*"

Ni matumaini yangu kwamba somo hili limekuwa la faida kwa wote. Zaburi hii ya ajabu hutuonyesha nguvu ya Mungu na msaada, ili kwamba tuweze kumtumainia na tusiruhusu dunia hii ituangushe. Hebu tufunge kwa kurudia kusoma mistari ya kwanza nay a mwisho ya Zaburi.

Zaburi 115:1, "*Ee BWANA kutukuza usitutukuze sisi, bali ulitukuze jina lako, kwa ajili ya fadhili zako, kwa ajili ya uaminifu wako.*" Zab. 115:18,"*Bali sisi tutamhimidi BWANA, tangu leo na hata milele.*"

Katika upendo wa Wakristo,

Ndg. Terry Warford